

Muundo wa Mashairi katika *Diwani ya Mnyampala (1965)* na Nafasi yake katika Kuibua Maudhui

Anna Nicholaus Kyamba

Ikisiri

Makala hii inachambua muundo wa mashairi katika *Diwani ya Mnyampala (1965)* na nafasi yake katika kuibua maudhui. Lengo ni kuangalia vipengele vya muundo vinavyojitokeza katika diwani hii. Vipengele vilivyoshughulikiwa ni mishororo, beti, mizani, vina, kituo au kibwagizo na mkarara. Pia, tunaangalia muundo huo ulivyotumika kuibua dhamira mbalimbali za kisiasa, kijamii na kiuchumi katika diwani hiyo. Makala hii pia inadadisi namna mbinu za kimuundo zilivyofanikisha usawiri na ubainishaji wa falsafa ya mtunzi kuhusu ushairi wa Kiswahili na nafasi ya ushairi katika jamii. Makala imeanza kwa kugusia usuli wa historia ya ushairi wa Kiswahili, historia fupi ya maisha ya Mathias Mnyampala na nadharia yake kuhusu ushairi wa Kiswahili. Data za makala hii zimepatikana kwa kusoma matini husika na kuchambua vipengele vyake vya kimuundo.

1.0 Utangulizi

Ushairi ni sanaa ya lugha ya mkato yenye ubunaji, inayosawiri na kuonesha au kueleza jambo, hisi au hali kwa namna yenye kuvutia hisia, katika mpangilio mahususi wa maneno fasaha na yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha, sitiari, katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo, ili kuleta wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisi fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo ... (Mulokozi na Kahigi, 1982:25).

Pamoja na ukweli wa fasili hii hata hivyo ina upungufu kidogo, kwani si kila shairi linagusa moyo. Ushairi ni utanzu wenye historia ndefu hususani katika fasihi ya Kiswahili, kama ambavyo Wamitila (2008b) anaeleza kwa kusema: “wataalamu wanakubaliana kuwa utanzu huu una historia ndefu”. Hata hivyo mpaka leo wataalamu mbalimbali wanadai kuwa hakuna makubaliano yaliyoafikiwa kuhusu utungo wa kwanza wa kishairi kuwa uliandikwa lini na mwandishi gani. Kutokana na haya tunaweza kusema, ushairi ni sanaa iliyobuniwa na mwanadamu katika karne mbalimbali za maisha zilizopita na kuendelea hata katika karne ya leo. Ushairi ulitumika na umeendelea kutumika kuelezea masuala ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii.

Katika karne ya 20 ya maendeleo ya ushairi mikabala miwili iliibuka; mkabala wa kimapokeo na mkabala wa kisasa. Katika kipindi hicho utanzu wa ushairi ulishughulikiwa na kuandikwa na waandishi wengi hali ambayo ilichochea kuwapo kwa kazi nyingi za ushairi wa Kiswahili. Kutokana na maendeleo hayo

kulitokea mgogoro wa ushairi wa Kiswahili uliofanya kuwepo kwa mitazamo au mikabala miwili. Mkabala wa kimapokeo ni ule unaozingatia urari wa vina na mizani kuwa ni uti wa mgongo wa ushairi. Miongoni mwa wafuasi wa mkabala huu ni Akilimali Snow White, Mathias Mnyampala, Saadan Kandoro, Amri Abedi, na Shaaban Robert. Na mkabala wa kisasa ni ule usiozingatia urari wa vina na mizani (Mulokozi, 1996). Miongoni mwa wafuasi wa mkabala huu ni Euphrase Kezilahabi, Kulikoyela Kahigi na Mugyabuso Mulokozi. Mgogoro wa ushairi ulichochea kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya kijamii pamoja na elimu ya kikoloni. Mgogoro huu ulikuwa zaidi baada ya Euphrase Kezilahabi kuandika diwani yake ya *Kichomi* (1974) ambayo mashairi mengi hayakufuata urari wa vina na mizani, jambo ambalo liliwakasirisha sana wanamapokeo. Kadhalika, wanamapokeo walisema kuruhusu ushairi wa kisasa kuwepo ni sawa na kuuu ushairi wa Kiswahili. Wanausasa pia walidai kuwa kuendelea kung'ang'ania kwamba vina na mizani ni uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili ni kuufanya ushairi wa Kiswahili kudumaa na kutopiga hatua yoyote ya kimaendeleo (Mulokozi, 1975). Kwa ujumla, mgogoro wa ushairi uliendelea na kufikia wakati ambapo kila upande uliushutumu upande mwingine kwamba unaua ushairi wa Kiswahili. Hii yote ilisababishwa na misimamo yao juu ya mtindo wa ushairi wa Kiswahili.

Kipindi hicho cha mgogoro Mnyampala¹ alikuwa amekwishafariki, hivyo hatuwezi kuzungumzia sana kama yeye angekubaliana na wanausasa au la. Tunachojua ni kwamba Mnyampala aliandika kazi zake kwa kugemea katika kanuni za kimapokeo za uandishi wa ushairi, ndio maana tunamuweka katika kundi la wanamapokeo. Kazi zake nyingi za ushairi alizoandika zilihusu ujenzi wa jamii mpya yenye usawa kwa watu wote. Kwa mfano, mashairi yake yaliyopo katika *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Ngonjera za Ukuta I* (1970) na *Ngonjera za Ukuta II* (1971) yanazungumzia ujenzi wa jamii mpya inayoheshimu haki za binadamu miongoni mwa wanajamii chini ya Azimio la Arusha. Mambo mengine aliyoyazungumzia ni misingi ya Azimio la Arusha, utekelezaji wake, mafanikio na upungufu wake. Katika makala hii, pamoja na utangulizi huu mfupi, sehemu nyingine za makala zinaongelea historia ya Mathias Mnyampala, hususani maisha na maandiko yake, nadharia ya Mnyampala kuhusu ushairi wa Kiswahili, muhtasari wa diwani ya Mathias Mnyampala, muktadha wa diwani hiyo, na muundo aliotumia mwandishi katika diwani yake na ulivyosaidia kuibua maudhui mbalimbali katika diwani hiyo. Mwisho kabisa ni hitimisho.

¹ Katika makala hii jina la Mnyampala na Mathias Mnyampala linamrejelea mtu mmoja. Alifariki mwaka 1969.

2.0 Historia ya Mtunzi Mathias Mnyampala

Historia ya Mathias Mnyampala tunaigawa katika sehemu mbili: maisha yake na maandiko yake ya fasihi ya Kiswahili.

2.1 Maisha ya Mathias Mnyampala

Kwa mujibu wa Madumulla (2011) na Issa (2013) Mathias Mnyampala ambaye kabla hajabatizwa aliitwa Emnzehe, alizaliwa tarehe 18, Novemba 1917 katika kitongoji cha Munhunya, kijiji cha Ihumwa, manispaa ya Dodoma. Baba yake aliitwa Mnyampala Machichimi, alikuwa mhunzi na baadaye mchungaji (alichunga ng'ombe). Mama yake aliitwa Odina Mbogoni. Mathias Mnyampala alipokuwa katika umri mdogo alipewa jukumu la kuchunga mifugo. Aliposikia habari za wasomi alifikiri ni kabila la watu waishio misheni. Mnamo mwaka 1927, Mathias Mnyampala alifanyiwa jando kwa mujibu wa mila na desturi za Kigogo.

Mathias Mnyampala alijiendeleva kielimu kupitia mfumo usio rasmi na kupata maarifa ya kusoma, kuandika na kuhesabu kupitia mafundisho ya dini aliyopata katika Kanisa la Katoliki. Pia, aliwahi kwenda *Mzumbe Local Government School* kusoma masuala ya sheria. Kwa kuwa elimu yake ilikuwa ya kubahatisha, ni vigumu kufahamu kiwango chake cha elimu alichofikia kwani hakuwahi kupata cheti cha kuhitimu darasa lolote (Madumulla, 2011). Mathias Mnyampala alioa wake watatu, Cecilia², Mary³ na Magreth⁴. Baada ya kubatizwa alilazimika kufunga ndoa ya mke mmoja kutokana na imani ya Kanisa Katoliki; mke huyo ni Mary Mangwela. Aliishi na mke huyu mpaka kifo chake. Alibahatika kupata watoto watatu, ambapo mmoja aliitwa Aloyce kutoka kwa mkewe Cecilia. Kwa mkewe Mary Mangwela walipata mtoto aitwaye Charles na kwa Magreth walifanikiwa kupata mtoto mmoja aliyetitwa Edward.

Katika kipindi cha mwaka 1936 hadi 1968, Mnyampala aliajiriwa na kufanya kazi mbalimbali ndani na nje ya mkoa wa Dodoma. Alikuwa mwalimu wa dini ya Katoliki katika kijiji cha Mzongole kilichopo Bahi. Baadaye alikuwa karani wa kodi wilayani Manyoni mkoa wa Singida. Pia aliwahi kuwa mwalimu katika vijiji vya Mpinga na Nthangano huko Dodoma. Baadaye akawa karani wa kodi huko Kinyambwa chini ya mtemi Makasi Hombolo kwa mtemi Mwaluko. Mwaka 1942 alipangiwa Makutupora chini ya mtemi Chitindi kama kituo chake cha kazi ya ukarani huku akisimamia ukusanyaji wa kodi Dodoma kwa mtemi Bilingi. kadhalika mwaka 1952 alipata kazi ya ukarani ya baraza la watemi wote chini ya mtemi Mazengo na kuwa katibu wa Mamlaka ya Wenyeji. Pia, alifanya kazi katika mradi wa utafiti wa ndorobo huko Shinyanga na pia alikuwa mtunza stoo. Baadaye alifanya kazi hiyo huko Manyoni mkoani Singida. Alifanya kazi katika

² Mke wa kwanza wa Mathias Mnyampala.

³ Mke wa pili wa Mathias Mnyampala.

⁴ Mke wa tatu wa Mathias Mnyampala.

mradi wa kilimo cha karanga wilayani Kongwa. Mwaka 1954 hadi 1955 alifanya kazi ya ukarani wa kupiga chapa katika mashamba ya Kimamba, Ilonga na Ludewa huko Kilosa, Morogoro. Vilevile alifanya kazi ya kuchapa katika idara ya maji mjini Dodoma na alikuwa diwani katika Halmashauri ya Mji wa Dodoma. Pia, alikuwa mjumbe wa Kamati ya Elimu ya Mkoa wa Dodoma. Mwaka 1960 hadi 1962 alifanya kazi ya uliwali na uhakimu huko Mpanda.

Mnamo mwaka 1963 hadi 1966 alifanya kazi katika mahakama ya mwanzo Temeke na baadaye Kariakoo mkoani Dar es Salaam akiwa mkuu wa mahakimu wengine. Mwaka 1966 alifanya kazi katika mahakama ya kadhi⁵ ya dini ya Kiislamu. Mwaka 1967, Mnyampala alifanya kazi Dar es Salaam katika Mahakama Kuu na kuwa mfasiri wa kazi za majaji. Mwaka 1968 alihamishiwa Dodoma kikazi na baadaye aliomba kustaafu kutokana na maradhi yaliyompata. Maradhi haya yalidumu mpaka umauti ulipomfika mnamo tarehe 8 Juni 1969. Kutokana na maisha yake haya na utendaji wa kazi yalimfanya kuandika kazi zake zilizoelezea masuala ya uchumi, utamaduni na siasa.

2.2 Maandiko ya Mathias Mnyampala

Mathias Mnyampala aliandika kazi nyingi katika ushairi na nathari. Kazi zake nyingi za ushairi na nathari zimesheheni matumizi ya lugha ya hekima kama anavyosisitiza mwenyewe katika ufafanuzi wa maana ya ushairi⁶. Katika mashairi alitunga mashairi ya utatu, unne, mtiririko, msisitizo, vidato na tenzi. Hata hivyo, ni kazi chache tu za Mnyampala ndizo zilizochapwa (Madumulla, 2011; Issa, 2013). Madumulla anasema kuwa kazi nyingi hazijachapwa na baadhi ya kazi hizo zipo katika hatua za awali za uchapishaji. Baadhi ya kazi alizochapisha ni: *Historia, mila na Desturi za Wagogo* (1954), *Kisa cha Mrina Asali na Wenzake Wawili* (1961), *Fasili Johari ya Mashairi* (1964), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965), *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Waadhi wa Ushairi* (1965), *Utenzi wa Zaburi* (1965), *Sikilizeni Hekima, Methali na Mawaidha* (1966), *Kito cha Hekima pamoja na Maelezo Sehemu ya Kwanza* (1966), *Kisa cha Bahati na Wazazi Wake* (1967) na *Utenzi wa Injili* (1967). Kazi nyingine ni *Mbinu za Ujamaa* (1968), *Ngonjera za Ukuta I* (1971), *Ngonjera za Ukuta II* (1972), *Historia ya Kiswahili* (1977) (alishirikiana na S. Chiraghdin), *Maisha ya Sheikh Amri Abedi Kaluta* (2011), *Maisha Kugharamia* (2014) na *Ugogo na Ardhi Yake* (2014). Vitabu ambavyo havijachapishwa ni *Mashairi ya Vidato*, *Azimio la Arusha na Maandiko Matakatifu*, *Historia ya Mtemi Mazengo*, *Taaluma ya Kiswahili*,

⁵ Ni mahakama iliyokuwa ikishughulikia migogoro na ustawi wa Waislamu kwa kuangazia mambo kama vile ndoa, talaka, mirathi, wosia, wakfu, malezi ya watoto na usuluhishi wa migogoro ya Kiislamu.

⁶ Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale (Mnyampala, 1965) katika dibaji yake.

Mahadhi ya Kiswahili, Hazina ya Kiswahili, Ufasaha wa Kiswahili na Kito cha Hekima Namba 1 na 2.

Mnyampala anawakilisha kundi la washairi wa kimapokeo waliosisitiza urari wa vina na mizani pamoja na utoshelevu katika ushairi wa Kiswahili. Katika makala hii tutahakiki kazi moja ya Mathias Mnyampala iitwayo *Diwani ya Mnyampala* (1965), kwa kuchambua mashairi yake katika kipengele cha muundo ili kubaini nadharia yake ya ushairi wa Kiswahili inavyosawiriwa katika diwani hiyo na namna muundo huo ulivyosaidia kuibua maudhui ya kazi yake.

3.0 Nadharia ya Mnyampala kuhusu Ushairi wa Kiswahili

Kutokana na maana zinazokuhusu nadharia, katika diwani hii tumeona kwamba Mnyampala alikuwa na mwongozo anaofuata katika utunzi wa mashairi yake. Kwa ujumla, mtunzi huyu alikuwa anafuata kaida za kimapokeo. Hili linajibainisha kwa kuangalia kazi zake kuhusu ushairi wa Kiswahili. Katika dibaji ya *Diwani ya Mnyampala* anaona ushairi umejegwa na vitu viwili mahususi ambavyo ni: “maneno ya hekima” na “sanaa yenyewe” (lugha ya mkato, nzito, yenye kunata na iliyoungwa kwa urari wa vina na mizani). Mnyampala anaeleza maana ya ushairi katika dibaji⁷ yake kuwa:

Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Ndicho kitu kilicho bora sana katika maongozi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyoungwa kwa urari wa mizani na vina maalumu kwa shairi. Shairi laweza kumliza mtu akatokwa na machozi kwa ajili ya mchomo wa hanjari la kuuwata moyo na maini kwa ule mchomo na mguso wa maneno ya shairi la mshairi bora. Vile vile, shairi jingine laweza kuuburudisha moyo mtu akafurahi akthari ya furaha na kujiona kuwa nayo heri mithili ya mtu aliye peponi. Shairi lina usemi ulio mtamu sana. Kwa maoni yanayopenya moyo yaliyo bora sana. Hivyo ushairi una sifa iliyo bora sana ulimwenguni na mafunzo yenye uadilifu na mazingira ya dunia yalivyo (Mnyampala, 1965).

Kutokana na dondoo hili tunapata wazo kuwa kwa mujibu wa Mathias Mnyampala miongoni mwa sifa za ushairi wa Kiswahili ni pamoja na shairi kutumia lugha ya Kiswahili ya kishairi isiyokuwa na maneno ya kashfa wala matusi. Pia, ushairi unapaswa kuwa na urari wa vina na mizani kamili zinazotakiwa katika ushairi wa Kiswahili. Sifa nyingine za ushairi wa Kiswahili anazobainisha mtunzi huyu ni kuwa shairi linapaswa liwe na vina vinavyopatana au vinavyolingana, hususani mwishoni mwa kila msitari kwa ubeti mzima, ingawa vina vya kati vinaweza kukosekana. Katika dibaji hiyo, Mnyampala anasisitiza juu ya sanaa ya shairi kwa kusema kuwa: shairi la Kiswahili lihusu mwendo wa mashairi bora, yaani linatakiwa lisizidi mno maneno ya kurudiarudia, lisitungwe namna ya kulinganisha

⁷ Katika kitabu nilichotumia Dibaji haijapewa ukurasa.

matuta; lisiwe pyororo la mashairi, bali liwe shairi kamili kama mashairi ya watu mahiri, werevu na wenye hekima. Mbali na sifa hizi za kimapokeo mtunzi huyu amependekeza sifa za ushairi ambazo si tu zinatakiwa katika ushairi wa kimapokeo bali pia hata katika ushairi wa kisasa. Sifa hii ni utoshelevu wa shairi. Anasema shairi lililo jema sana ni lile linalotosheleza haja ama kusudi la kisa cha mtunzi. Kwa hiyo urefu au ufupi wa shairi hutegemea kisa cha mtunzi, ikiwa kisa cha mtunzi ni kifupi basi hata shairi litakuwa fupi na ikiwa kisa cha mtunzi ni kirefu kadhalika shairi litapaswa kuwa refu (taz. dibaji ya *Diwani ya Mnyampala*, 1965).

Kimsingi Mnyampala anaungana na wataalamu wengine wa ushairi waliokuwapo kipindi hicho kama Saadan Kandoro, Amri Abedi na Shaaban Robert na wengineo wengi. Hata hivyo, mbali ya kuwa mawazo ya wataalamu hawa kuhusu ushairi ni mazuri bado kuna baadhi ya hoja zao hazijatengemaa. Kwa mfano, mkabala wa kimapokeo anaouwakilisha Mnyampala kuhusu ushairi unatufanya tuone utunzi wa mashairi kama jambo gumu kwani ushairi umetazamwa kama ni kitu kitukufu sana na watu wawezao kutunga nao sharti wawe hivyo hivyo. Kwa maneno mengine, wanamapokeo wameelekea kuutukuza mno utanzu wa ushairi. Pili, ikiwa ushairi ni maneno ya hekima, je hekima ni nini na inapimwaje? Hivyo maswali haya yatakapopatiwa majibu pengine ndipo suala la hekima linaweza kuwa kigezo kizuri cha kutathminia utunzi na ubora wa sanaa yenyewe ya ushairi wa Kiswahili (ingawa si lengo la makala hii kuyajibu).

Mnyampala na nadharia yake ya ushairi inalenga mashairi ya kijadi na anasisitiza sana maneno ya hekima na sanaa yenyewe kama vile lugha na mpangilio wa vina na mizani. Pia, anasisitiza kuwa hata kama shairi halina vina basi liwe na mtiririko na muwala, pia kuwe na maana bora sana yenye mafundisho ndani mwake, ufurahisho, mvuto wa maarifa ama kasida za kumsifu Mungu, pengine watu maarufu au vitu vinginevyo vinavyostahili kusifiwa. Swali la kujiuliza hapa ni kwamba je, hiyo ndiyo maana ya ushairi? Tuonavyo sisi ushairi ni utungo wa kawaida kama zilivyo tungo nyinginezo ambazo kifani hujipambanua kwa kuundwa na matumizi ya lugha kimantiki ambapo maneno machache huweza kutumiwa kuwasilisha mambo mengi na kimaudhui; utungo wa ushairi unaweza kuhusu jambo lolote linalohusiana na tajiriba za watu wa jamii inayohusika. Baada ya kuangalia nadharia yake, tuone muhtasari wa diwani yake.

4.0 Muhtasari wa *Diwani ya Mnyampala*

Diwani ya Mnyampala ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1965 na kampuni ya uchapishaji ya *East African Literature Bureau*. Diwani hii ina jumla ya mashairi 178 ambayo yamegawanywa katika sehemu nne. Ni diwani ambayo kwa kiasi kikubwa imesheheni mashairi yanayofuata kanuni za ushairi wa kimapokeo yaani kufuata kanuni za urari wa vina na mizani, ujumi wa lugha na idadi ya mistari hususani unne; kwa kutaja chache tu, isipokuwa mashairi ya 139

hadi 147. Maudhui ya diwani hii yanahusu masuala mbalimbali yanayoibuka katika jamii na nyanja za maisha ya mwanadamu kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Gibbe (1978) anabainisha baadhi ya mambo yaliyoshughulikiwa katika *Diwani ya Mnyampala* kuwa ni siasa, maadili, dini, ukoloni na harakati za kudai uhuru na haki miongoni mwa wanajamii. Kwa kutumia nadharia yake ya kimapokeo tunachambua matumizi ya muundo katika diwani hiyo. Matumizi ya muundo yanaendana na muktadha uliokuwapo wakati huo. Hivyo katika sehemu ifuatayo tunaelezea kwa ufupi muktadha wa diwani husika.

4.1 Muktadha wa Diwani ya Mnyampala

Muktadha ni mazingira ya kihistoria, kijiografia, kisiasa, kiuchumi, kijamii au ya kiutendaji yaliyozua utungo husika. Muktadha pia hurejelea mambo yaliyomzunguka mwandishi wakati wa utungaji wake na kufichua masuala muhimu ya kazi ya fasihi katika viwango vya fani na maudhui. Aidha, kupitia muktadha wa utungaji, mhakiki huelewa dhamira za mtunzi husika kupitia kazi yake (King'ei na Kemoli, 2001; Njogu na Chimera, 2011). Naye, Wamitila (2010) anaeleza kuwa uchambuzi wa kazi ya kifasihi hutegemea muktadha kwa kiasi kikubwa.

Diwani hii ilitungwa miaka ya sitini mara baada ya Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961. Utungwaji wake ulichochea na masuala ya uongozi na utawala, kuanzishwa kwa vyama vya kisiasa, matukio ya kihistoria kama vile muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar (1964) na sera ya Ujamaa na Kujitegemea (1967). Vilevile, kazi hii ilitungwa na mtunzi ambaye kihistoria ni mwanasiasa na ni mchapa kazi. Kama asemavyo Mulokozi (1975), Mnyampala alikuwa mshairi maarufu kuliko wote baada ya Shaaban Robert mpaka alipofariki mwaka 1969. Vilevile, Mnyampala katika kipindi cha uhai wake alikuwa mwanaharakati katika masuala mbalimbali. Miongoni mwa masuala hayo ni yale yanayohusiana na uhuru, muungano, siasa ya ujamaa na kujitegemea. Kwa mfano, shairi namba 166 lisemalo 'Uhuru Uwe wa Kheri' na namba 169 'Muungano Utupambe'. Utunzi wa diwani hii ulichangiwa na muktadha wa kihistoria na kijamii pamoja na maisha ya mtunzi wa diwani hii na kazi alizozifanya wakati wa uhai wake ndani na nje ya mkoa wa Dodoma⁸.

Kutokana na hayo yote ushairi ulitumika na unaendelea kutumika kuelezea masuala ya kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii kama asemavyo Kitogo (2002) kuwa wataalamu wa fasihi na wale wa sayansi ya siasa wanakubali kwamba masuala ya kisiasa yana mchango mkubwa katika kuonyesha utokezaji wa mambo mengine yanayohusiana na uchumi, utamaduni na maisha ya jamii. Mfano wa mashairi ya Mnyampala yanayosadifu muktadha huo ni shairi namba 106 lenye

⁸ Taz. katika historia ya mwandishi katika makala hii.

kichwa ‘Madaraka Tumebeba’ (uk. 91) na shairi namba 163 ‘Uhuru una Kiungo’ (uk. 143). Kutokana na miktadha hiyo ndipo tunapata fani na maudhui ya *Diwani ya Mnyampala* ambapo hasa makala yetu inamakinikia muundo kama mojawapo ya vipengele vya fani.

5.0 Uchambuzi wa Muundo katika *Diwani ya Mnyampala*

Senkoro (1982) anafafanua kwamba fani huelezewa kama umbo la nje la kazi ya fasihi akimaanisha kuwa ni ufundi wa kisanaa anaotumia mwandishi wa kazi ya fasihi. Katika diwani hii tunachambua matumizi ya muundo kama kipengele cha fani, Muundo ni istilahi inayotumiwa kurejelea jumla ya uhusiano unaokuwako kati ya vijishehemu mbalimbali vinavyounda kitu kamili au cha jumla (Wamitila, 2003). Njogu na Chimera (2011) wanadai kuwa kuna miundo mingi katika ushairi wa Kiswahili. Vipengele vingi vinavyotumika kama sehemu ya muundo ni mishororo (mistari), beti, mizani na vina. Wanafafanua kuwa urefu wa mshororo hutegemea idadi ya mizani au mtiririko wa mawazo kama ni shairi-huru. Urefu wa beti nao unategemea idadi ya mistari katika kila ubeti. Kwa mujibu wa Mulokozi (1989) mashairi ya Kiswahili yana miundo mingi. Vilevile, Samwel na wenzake (2013) wanafafanua muundo kuwa hudhahirika kwenye umbo la shairi. Wanadai umbo ni sura ya nje ya shairi au kazi ya sanaa ni jinsi shairi husika linavyoonekana. Wanaongeza kuwa muundo wa shairi hutegemea mkabala wa mshairi husika, ikiwa ni wa kimapokeo au wa kisasa. Hivyo basi, muundo wa ushairi ni mjengo au mpangilio wa kazi ya ushairi. Aidha, wataalamu hawa wanabainisha vipengele vya muundo wa ushairi kuwa ni beti, mshororo, vipande, mizani, vina, kibwagizo, mkarara na kituo au kimalizio.

Ni jambo la muhimu kujadili muundo wa shairi kwa kuwa kimaudhui muundo huweza kuathiri mtiririko wa maana ya shairi. Vipengele vya kimuundo ambavyo tunavijadili katika makala hii ni beti, mshororo, vipande, mizani, vina, mkarara na kituo au kimalizio na namna vinavyoibua maudhui (dhamira) mbalimbali katika diwani husika. Uchambuzi wake ni kama ifuatavyo:

5.1 Beti

Beti ni jumla ya mistari yenye wazo moja linalojitosheleza. Samwel na wenzake (2013) wanaeleza kuwa beti ni mkusanyiko wa mistari au mishororo na kwa kawaida huwa na wazo moja kamilifu. Kwa ujumla katika uchambuzi tunaangalia endapo shairi husika lina beti au halina pamoja na muundo wa beti hizo. Kwa upande wa *Diwani ya Mnyampala* mtunzi ametumia muundo wa kimapokeo ambapo takribani mashairi yake yote yana beti zenye mistari au mishororo minne inayojitosheleza. Kuna mashairi yenye beti nne, kwa mfano shairi la ‘Ndoa Akiridhi Nani’ (uk. 4) lenye dhamira ya wosia kwa wazazi, mapenzi na ndoa. Mshairi anawataka wazazi wasiwachagulie watoto wao wanaume au wanawake wa

kuwaoa, kinachotakiwa ni mapenzi ya dharti kwa wawili waoanao. Pia, shairi la ‘Hima Hima Islamu’ uk. 6 –7, katika shairi hili mshairi anahimiza watu kuwa waaminifu kwa Mungu wao hasa kwa Waislamu wakati wa mfungo wa Ramadhani. Hivyo shairi hili linahusu dini, ambapo mtunzi anawahimiza Waislamu kufunga mwezi wa toba kama dini yao inavyotaka.

Mashairi mengine yenye beti nne ni ‘Nashangilia Unguja’ uk. 24, ‘Kukuzwa Twafurahia’ uk. 38, ‘Bingwa Anapokwambia’ uk. 42, ‘Siyo Ngano ni Shayiri’ uk. 53, ‘Taarifa Tultuma’ uk. 70 -71. ‘Ni Nani Hasa wa Ubaya?’ uk. 141-142 na ‘Uhuru una Kiungo’ uk. 143. Pia, kuna mashairi yenye beti tano, mfano ‘Panya Simwonjeshe Pamba’ uk. 52; sita, mfano ‘Mwaka na uwe wa Heri’ uk.5; saba, mfano ‘Mgema Ukimsifu’ uk.26; nane, kama vile ‘Tumefika Salama’ uk.106; tisa, mfano ‘Nikaze Yangu Nira’ uk. 122; kumi, mfano ‘Yaliyopita Yamepita’ uk.120; kumi na moja, mfano ‘Si Bure ni Chokochoko’ uk.118; na kumi na mbili, mfano ‘Bahari Kuwaka Moto’ uk. 110-111. Kadhalika yapo mashairi yenye beti kumi na tatu mfano shairi la ‘Ukungu Kaziba Mbele’ uk. 22 na kuna shairi lenye beti kumi na nne mfano shairi la ‘Binadamu haridhiki’ uk. 28 na mengineyo.

Beti zote za Mnyampala alizoandika katika diwani hii zinajitosheleza. Mnyampala, kama mfuasi wa wanamapokeo, anaona utoshelevu wa shairi kwake hutegemea vijenzi vyake ambavyo ni pamoja na urari wa vina na mizani, urefu au ufupi wa beti, idadi ya mishororo na kituo. Mashairi yote katika *Diwani ya Mnyampala* yana utoshelevu katika viwango tofauti tofauti yaani upo utoshelevu katika kiwango cha mshororo kukamilisha beti na beti kukamilisha shairi zima na mwisho shairi zima kukamilisha wazo au kusudi la mtunzi. Suala hili la utoshelevu hutupatia pia muwala wa shairi.

Vilevile, Mnyampala alikuwa mbunifu kwani aliweza kuunda beti nyingine zenye muundo tofauti na ule tuliozoea wa mistari minne. Pia aliyaita mashairi haya ni mashairi ya msisitizo, ambapo alikuwa anasitiziza watu kufuata haki za binadamu, kuachana na dhuluma, na madhara ya dhuluma hiyo.

5. 2 Mizani

Mizani ni vipimo maalumu vya urefu wa mstari wa ushairi vinavyogawanywa katika silabi za kila neno. Na kila silabi moja ni mizani moja (Mayoka, 1984). Kwa upande mwingine Njogu na Chimerah (2011) wanaeleza kuwa mizani ni hesabu ya silabi katika kila neno. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa mizani ni jumla ya silabi katika neno, kipande au mshororo mmoja. Kwa wanamapokeo mshororo mmoja unatakiwa uwe na mizani kumi na sita na kipande au nusu mshororo huwa na mizani nane. Kwa mfano shairi la kwanza ‘Usifurahi mwanzoni’, msanii anasema:

Wangapi wadanganyika, na furaha za mwanzoni?
Maneno wakiropoka, kucheka wenye huzuni,

Mwisho ulipowafika, na kufa walitamani,
Usifurahi mwanzoni, hadi ufike mwishoni.
(uk. 1 ubeti wa 9)

Katika shairi hili kuna mizani 16 kwa msitari au mshororo mzima na mizani nane (8) kwa nusu mshororo (kipande). Tazama uchanganuzi wa kielelezo hapa chini:

Wa	nga	pi	Wa	da	nga	nyi	ka	**	Na	Fu	ra	ha	za	Mwa	nzo	ni?
1	2	3	4	5	6	7	8		9	10	11	12	13	14	15	16

Katika kielelezo hiki alama ** imetumika kuonyesha mpaka kati ya nusu moja na nusu nyingine za mishororo ya ubeti wa shairi na kwamba nyuma ya alama hii kuna mizani 8 hali kadhalika mbele ya alama hii kuna mizani 8. Kwa ujumla mashairi yote ya mashairi huyu yana ulinganifu wa mizani kwa mshororo mzima au nusu mshororo. Hapa maneno yaliyopo katika mishororo yametumika kuibua dhamira mbalimbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kupitia muundo wa mishororo yake mtunzi ameweza kuonyesha uwezo wake wa matumizi ya lugha na ameweza kutosheleza haja ya utunzi wake kwa kuibua maudhui mbalimbali yanayohusu uongozi, unyonyaji, waandishi, mapenzi, ndoa, uzalendo na mengineyo. Hii ni kwa sababu muundo na maudhui ni vitu vinavyotegemeana, huathiriana na kukamilisha. Mpangilio mzuri wa mawazo huwezesha maudhui mbalimbali kuwafikia walengwa waliokusudiwa. Baada ya kuangalia muundo wa beti sasa tuone jinsi alivyopangilia vina katika mashairi yake.

5.3 Vina

Vina ni silabi za namna moja zinazotokea baada ya kila mizani kadhaa katika mstari wa shairi, katika ushairi wa kimapokeo kuna vina vya kati na mwisho vina ambavyo huwa na ulinganifu wa namna fulani. Samwel na wenzake (2013) wanasema kuwa vina ni silabi zinazofanana katika mshororo wa shairi au beti. Wanatoa maelezo zaidi kuwa kuna aina nyingi za vina ambazo ni pamoja na kina cha kati, kile kinachotokea katika kila kipande cha mshororo ambacho si cha mwisho na kina cha mwisho ambacho hujitokeza katika kipande cha mwisho cha mshororo. Mtunzi wa diwani hii ametumia vina vinavyolingana kwa kila kipande kwa kiasi kikubwa. Mnyampala anasema katika dibaji yake kuwa shairi bora ni lile lililohitilafiana vina. Vina vya kati mbali na vina vya mwisho hupendeza masikioni mghani anapoimba. Hili limejidhihirisha wazi wazi katika mashairi yake. Kwani katika kila shairi kuna ulinganifu wa vina angalau katika kila ubeti, na mahali pengine kina cha mwisho au cha kati hubakia kuwa kimoja katika shairi zima. Mfano shairi ‘Mali Mfano Maua’, uk. 11- 14, kuna vina vya kati ‘ka’ na vina vya mwisho ‘a’ kwa ubeti wa kwanza hadi wa tatu. Kuanzia ubeti wa nne vina vimebadilika, ambapo vina vya kati vimekuwa ‘ko’ na mwishoni ‘ki’. Pia katika

kibwagizo mistari mitatu ya mwanzo kina cha kati ni ‘a’ na mwisho ni ‘ka’. Mundo huu wa kufanana kwa vina katika kila ubeti wa shairi Mnyampala aliuita muundo wa mtiririko. Muundo huu aliumudu vyema katika utunzi wake wa mashairi.

Mathalani, katika shairi la ‘Usifurahi Mwanzoni’ uk. 1, ubeti wa kwanza na wa pili una kina ‘ie’ na ‘ni’. Aidha, kila ubeti wa shairi hilo una vina vya kati ‘ka’ na vina vya mwisho ‘a’. Vina vinavyobadilika katika shairi hili hasa ni vina vya kati lakini kina cha mwisho kimebaki kuwa kilekile. Hivyo katika shairi hilo kuna vina vya kati nda, ka, ma, li, ee, ni, ka na zi. Hivyo katika shairi hilo vina vya kati vimebadilika lakini kina cha mwisho kimebaki kuwa kilekile ambacho ni ‘ni’. Hii inaonyesha mwandishi alitunga kwa kufuata kanuni za ushairi zilizoandikwa na Abedi (1954) anayedai kuwa kwa desturi vina vya silabi ya nane kwa desturi inayotumika sana huwa tofauti kati ya ubeti mmoja na mwingine. Naye, Mnyampala katika dibaji yake anasema kuwa shairi bora ni lile linalohitilafiana vina. Vina vya kati vinapotofautiana na vya mwisho shairi hupendeza masikioni mghani aimbapo. Kwa mfano, ubeti namba tisa kina cha kati ni ‘ka’ na ubeti namba kumi kina cha kati ni ‘zi’ lakini kina cha mwisho katika ubeti wa tisa na kumi kinakuwa kilekile ambacho ni ‘ni’ kama inavyoonekana hapa chini:

Wangapi wadanganyika, na furaha za mwanzoni?
Maneno wakiropoka, kucheka wenye huzuni,
Mwisho walipofika, na kufa walitamani,
Usifurahi mwanzoni, hadi ufike mwishoni (ubeti wa 9).

Tamati masimulizi, furaha paka mwishoni,
Katikati utatizi, kuna misiba njiani,
Shabaha za pingamizi, zitakutoa rahani,
Usifurahi mwanzoni, hadi ufike mwishoni (uk. 1 ubeti wa 10).

Hivyo basi, shairi hili lina ulinganifu wa vina kwa kila ubeti, mshororo au kipande, na hali hii ndiyo inayotawala mashairi yake yote. Wamitila (2003) anafafanua vina kuwa ni dhana inayotumiwa katika taaluma ya ushairi kuelezea silabi zinazofanana katika sehemu sawa katika mpangilio wa ubeti wa shairi. Hivyo katika mashairi ya Mnyampala amefuata urari wa vina na mizani ili kuleta upangilifu wa msamiati na sauti katika kukamilisha maana kwa njia bora zaidi katika kuelimisha na kufurahisha hadhira. Abedi (1954) katika utangulizi wake anafafanua kuwa vina vya beti zao vinawaletea maneno wanayolazimika kuyatafuta katika lugha kujua maana sahihi. Na hivyo elimu yao juu ya lugha huongezeka na kwa kadiri waendeleavyo wanakuwa wepesi kutunga na kujifunza wapatayo. Naye, Mnyampala katika dibaji yake anaamini kuwa mtu yeyote anavyotunga mashairi kwa kuzingatia upatanifu wa vina hasa mwishoni husaidia kukuza lugha husika. Kwa ujumla mawazo ya mtunzi yanatusaidia kupata vina. Hivyo kutokana na vina

tunaweza kujua maudhui yaliyopo katika utungo husika. Kama asemavyo Abedi (1954) kuwa mawazo ya mtungaji yazue vina na wala sio vina kuzua mawazo. Anaongezea kuwa vina vinavyohitilafiana vinafanya shairi lichapukie na kumzindua msomaji na msikilizaji kila wazo jipya linalojitokeza pamoja na kina kipya. Hivyo vina kipya husaidia kubaini maudhui mapya yanayojitokeza katika shairi au mashairi. Pia vina vilivyopangiliwa vizuri vinasaidia maudhui kueleweka na shairi kuvutia.

5. 4 Mistari au Mishororo

Kuhusu muundo wa idadi ya mishororo katika kila ubeti, inaonyesha kuwa mashairi mengi katika diwani hii yamejengwa kwa muundo wa tarbia (mashairi yaliyoundwa katika mjengo wa mishororo minne katika kila ubeti, pia huitwa mashairi ya unne). Kwa kuwa si rahisi kunukuu kila shairi, tutatoa mfano wa shairi la ‘Usifurahi mwanzoni’ ambalo ni la tarbia kama ifuatavyo;

Wangapi wadanganyika, na furaha za mwanzoni?
Maneno wakiropoka, kucheka wenye huzuni
Mwisho ulipowafika, na kufa walitamani
Usifurahi mwanoni hadi ufike mwishoni (uk. 1 ubeti wa 9).

Huu ni muundo uliotumika kwa kiwango kikubwa katika diwani hii kuibua maudhui mbalimbali ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Aidha, mbali na muundo huu kuna mashairi mengine yaliyojengwa kwa kutumia mishororo mitano na nusu. Kwa kawaida muundo huu hujulikana kama muundo wa mashairi ya msisitizo ambao aliuanzisha Mnyampala; mwenyewe anatamka kuwa anaweka msisitizo katika shairi la ‘Natunga Msisitizo’ uk. 121. Mnyampala anayaita mashairi hayo ni yenye mwendo mpya na ameyatambulisha kuwa ni mashairi yenye kufuata muundo wa mtiririko na msisitizo, katika diwani hii mashairi ya namna hii yanapatikana katika kurasa za 123 hadi 130. Nayo ni pamoja na ‘Natunga Msisitizo’ uk. 121, ‘Nikazie Yangu Nira’ uk. 122, ‘Lugha Yetu Kiswahili’ uk. 123, ‘Mawaidha ya Dunia’ uk. 124, ‘Naacha Vivyo Vilivyo’ uk. 126, ‘Hakuna Mkamilifu’ uk. 127, ‘Apendaye Kudhulumu’ uk. 128, ‘Mungu Ondoa Tatizo’ uk. 129, na ‘Amezaliwa Mwokozi’ uk. 130. Katika mashairi haya kuna mishororo 5 na nusu, ambapo kila ubeti una kipande cha msitari au mshororo kilichopachikwa katikati ya mstari wa pili na wa tatu. Mfano shairi la ‘Mungu Ondoa Tatizo’ ubeti wa kwanza unaosema:

Jirani wanagombana, kutwa kucha ni mizozo,
Kwani hawana patano, wagomba mfululizo,

Hawaishi mikwaruzo;⁹
 Mikwaruzo mashindo, kuonyeshana uwezo,
 Hawatamani **mwungano**, ambao kwao ni nguzo,
 Mola ondoa mizozo, majirani wafaulu (uk. 129 ubeti wa 1).

Kimundo ubeti huu una mishororo mitano na nusu. Katika shairi hili mwandishi anawasilisha maudhui mbalimbali yanayohusu uhusiano wa binadamu na Mungu (dini), masuala ya kisiasa (muungano), umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii, umuhimu wa lugha ya Kiswahili na masuala ya utamaduni wa jamii. Ingawa mtunzi kauita muundo huu muundo wa mashairi yenye mwendo mpya, msisitizo na mtiririko, lakini bado tunaona kuwa kuna urari wa vina na mizani. Lakini kwa upande mwingine ni muundo mpya tofauti na miundo waliyokuwa wanaandika washairi wenzake. Kwa ujumla mashairi ya msisitizo, kama yalivyotajwa hapo juu, yana umbo la kipekee, tofauti na maumbo ya mashairi tuliyoazoea. Upangilifu wake hulifanya shairi lipendeze na kuleta ladha kwa wasomaji wake. Ukichunguza mashairi ya msisitizo unabaini kuwa mashairi yote ya msisitizo ni mashairi ya mtiririko, kila ubeti una kipande cha mstari kilichopachikwa katikati ya msitari wa pili na wa tatu katika kila ubeti, neno la mwisho katika kipande cha tano ambacho ndicho huleta msisitizo, na pia ni kianzio cha msitari unaofuata yaani msitari wa tatu unaofuata, na lazima liwe nomino.

5.5 Kituo

Kipengele kingine cha kujadili katika kuhakiki muundo wa mashairi ni kituo¹⁰. Kituo ni ule mshororo wa mwisho katika kila ubeti wa shairi (Abedi, 1954). Abedi anaeleza kuwa kituo huweza kuwa kimalizio endapo mstari wa mwisho wa kila ubeti unabadilikabadilika. Pia, kituo kinaweza kuwa kibwagizo endapo mshororo wa mwisho wa ubeti unarudiwarudiwa (taz. pia Njogu na Chimerah, 2011). Hata hivyo jambo la msingi ni kuwa katika hali yoyote ile kituo ni nyenzo muhimu ya utungo wa mashairi kwa kuwa husaidia kuunganisha mawazo na kufupisha taarifa mara moja na kwa haraka zaidi. Mtunzi bora wa mashairi sharti afahamu namna nzuri ya kuitumia nyenzo hii. Katika mashairi ya *Diwani ya Mnyampala*, mtunzi ametumia vituo vya aina mbili; kituo kinachobadilikabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine na kituo ambacho hakibadilikiabadiliki kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Lengo la kibwagizo¹¹ (kituo ambacho hakibadiliki) ni kuisisitiza ujumbe uliopo katika ushairi husika. Kadhalika, Samwel na wenzake (2013) wanaeleza kuwa dhima ya kibwagizo katika shairi ni kumalizia ubeti na kushadidia dhamira

⁹ Huu ni nusu mshororo ambao una mizani pungufu kuliko mishororo mingine iliyo kamili. Nusu mshororo huu una mizani 8.

¹⁰ Kituo katika ushairi hufahamika pia kama kimalizio au kibwagizo.

¹¹ Vilevile kibwagizo huitwa kiitikio.

au wazo la shairi. Vina pia huwezesha kumtambulisha msanii, maudhui yake na shairi lenyewe. Dhima nyingine ya kibwagizo ni kurahisisha uwasilishaji wa shairi na kufanya mashairi yaimbiki.

Aidha, kituo kinachobadilikabadilika huashiria upana na mawanda ya mawazo ya msanii na kuufanya ushairi mzima uwe na utoshelevu uliotokana na muunganiko wa mawazo tofauti tofauti. Mashairi haya ni pamoja na ‘Washairi Tuna Huzuni’ uk. 150. Katika shairi hili kuna vituo tofautitofauti kama vile: ‘Watunzi tu msibani, tumepatwa na huzuni’ ubeti wa 5, na ‘Kifo cha Bwana Shaaban, kimetutia huzuni’ ubeti wa 1, 2, 3 na 9, ‘Mola muweke peponi, mpenzi wetu Shaaban’ ubeti wa 4 na 10, na ‘Mijini hata shuleni, watunzi tuna huzuni’ ubeti wa 8. Ingawa kituo katika shairi hili hubadilikabadilika, bado dhima yake ni kusisitiza jambo moja lilelile linalobeba maudhui ya kuonyesha huzuni ya kifo cha mtunzi mashuhuri wa ushairi ambaye ni Shaaban Robert aliyefariki mwaka 1962.

Aina nyingine ya kituo iliyotumika katika mashairi haya ni kituo kikuu kisichobadilikabadilika hasa katika kuonyesha uzito na kiini cha maudhui ya shairi husika. Maudhui hayo yanahusu malezi, wosia kwa watunzi kuhusu namna ya kutunga mashairi, uongozi, mapenzi, siasa, kipato na mengineyo. Haya ni pamoja na mashairi yafuatayo: ‘Usifurahi Mwanzoni’ uk. 1, kituo ni ‘Usifurahi mwanzoni, hadi ufike mwishoni’; pia shairi la ‘Kibaya kina Mwenyewe’ uk. 1, kituo chake ni “Kibaya kina wenyewe, ingawa chanuka shombo”; shairi la ‘Tungeni Mtiririko’ uk. 5 kituo ni “Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu” na shairi la ‘Mali Pepo na Dunia’ uk. 7 lenye kituo “Mali pepo ya dunia, yambatane na imani” yana vituo visivyobadilika. Kwa ujumla katika diwani hii kituo kisichobadilika kimetamalaki takribani katika mashairi yote.

5. 6 Mkarara

Mkarara ni urudiaji wa maneno unaojitokeza katika ushairi. Kwa mujibu wa Mutembe (2012) anafafanua kuwa mkarara ni ujirudiaji wa sauti, neno, maneno, sentensi, ama muundo uleule, bila kujali sehemu au nafasi ya ujirudiaji huo unapotokea. Hivyo, katika *Diwani ya Mnyampala* pia kuna ujirudiaji wa sauti, neno, maneno, sentensi na hata muundo wa beti husika katika takribani mashairi yote. Kutokana na fasili ya mkarara ya Mutembe tunaweza kusema kuwa vina vyote vinavyofanana katika ubeti wa shairi ni mkarara. Pia, vituo vyote na maneno yanayojirudiarudia ni mkarara. Mfano katika shairi la ‘Taabu kwa GUOGUO’, kuna ujirudiaji wa silabi ‘ao’ na ‘ni’ kwa kila ubeti. Pia, kuna urudiaji wa neno ‘guoguo’ ndani ya ubeti na hata ubeti hadi ubeti, kama tuonavyo ubeti huu:

Wamepangwa jina lao, Guoguo mitaani,
Na nguo wazibebao, hodi hodi majumbani,
Je huko kwenu mnao, wakopeshao mijini?
Heri nishone dukani, taabu kwa Guoguo.

Katika ubeti huo na baadhi katika shairi hilo kuna vina vya kati vinavyojirudia na vina vya mwisho wa ubeti. Zaidi, kuna ujirudiaji wa neno guoguo. Vilevile, kuna ujirudiaji wa mstari wa mwisho wa kila ubeti ili kuisisitiza maudhui yaliyomo katika shairi husika. Kwa namna nyingine, kuna ujirudiaji wa wazo zima na fikra ya biashara ndogondogo hususani za nguo wanazotembeza watu majumbani. Ujirudiaji huu unasisitiza kiini cha shairi husika. Hivyo, shairi hili linaasisitiza biashara ya mitumba au biashara ya umachinga, ambapo wauzaji wanakopesha lakini wakianza kudai wanadai kwa fujo. Hivyo anajaribu kuwaasa wanajamii kuepukana na mikopo ya nguo, mtunzi anawasihi watu kushona na kulipa kidogo kidogo. Hapa anasisitiza jamii kuchagua vitu vilivyo bora na vya thamani na wala wasikimbilie urahisi wa mambo. Kabla ya kufanya jambo lolote lazima kutafakari na kutathimini kwanza.

6.0 Hitimisho

Diwani ya Mnyampala imesawiri vyema nadharia ya kimapokeo kwa kuzingatia kanuni za ushairi zinazosisitiza urari wa vina na mizani na utoshelevu. Pia ametumia lugha nzuri isiyo na matusi yaani lugha ya hekima ambayo ni falsafa yake kuzingatia lugha fasaha isiyo na matusi. Utunzi wa *Diwani ya Mnyampala* unaonyesha kiwango cha hali ya juu kabisa cha kupevuka kwa msanii kifikra na kiutendaji. Kifasihi mtunzi huyu ameweza kuhuisha na kuweka misingi juu ya nadharia ya kijadi ya ushairi, mithili ya alivyofanya Amri Abedi (1954) ambaye aliandaa na kutoa mwongozo wa fani ya sanaa ya ushairi. Sawa na alivyofanya Mnyampala katika dibaji ya diwani hii amesisitiza umuhimu wa kanuni za ushairi¹² kama vile muundo na lugha. Mnyampala sawa na walivyofanya watunzi kama vile Shaaban Robert amechangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza lugha ya Kiswahili. Halikadhalika, mtunzi amebuni miundo mipya ya mashairi ya Kiswahili kama vile mashairi ya msisitizo na mashairi ya mtiririko. Wamitila (2010) anasema mashairi ya mtiririko huwa na vina vya ndani au ukwapi vinavyofanana katika utungo mzima. Ingawa miundo hii haijazikonga sana nyoyo za wapenzi wa sanaa ya ushairi lakini mpaka leo tungo za kimsisitizo na mtiririko kama alivyoziasisi mtaalamu huyu bado zipo na watunzi wanaweza kutumia katika utunzi wa mashairi. Hii inadhihirisha kuwa mchango wa Mathias Mnyampala katika sanaa na maendeleo ya ushairi wa Kiswahili hauna kifani.

¹² Kanuni hizo zilikwishajadiliwa katika utangulizi wa makala hii (uk 2).

Marejeleo

- Abedi, K.A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Gibbe, A.G. (1987). "Mathias Mnyampala-Mshairi Maarufu wa Kiswahili" katika *Mulika* Na.13. Dar es Salaam: TUKI, kur. 29-35.
- Issa, I. (2013) "Usawiri wa Mhusika Mwanamke katika Ushairi wa Mathias Mnyampala: Mifano kutoka *Diwani ya Mnyampala (1965) na Waadhi wa Ushairi (1965)*". Tasnifu ya Digrii ya Umahiri. Chuo kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Kezilahabi, E. (1974) *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
- King'ei, K. & Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
- Kitogo, S.A. (2002). "The Poet's Contribution to Political Development: A Case Study of Abdu Kandoro". Unpublished M.A. Dissertation. UDSM.
- Madumulla, J.S. (2011) "Mathias Mnyampala: Jabali Lililosahaulika." Makala iliyowasilishwa katika kumbukizi ya Amri Abedi na Mathias Mnyampala (Karimjee, Dar es Salaam). Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Mayoka, J.M. (1984). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mnyampala, M. (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Dar es Salaam: Kenya Literature Bureau
- _____ (1970). *Ngonjera za UKUTA: Kitabu cha Kwanza*. Dar es Salaam: Kenya Literature Bureau.
- _____ (1971). *Ngonjera za UKUTA: Kitabu cha Pili*. Dar es Salaam: Kenya Literature Bureau.
- _____ (2014). *Maisha ni Kugharimia*. Roy, M. (mhr). Paris: Bluu Pupliching.
- Mulokozi, M.M. (1975). "Revolution and Reaction in Swahili Poetry" in *Kiswahili Vol.* 45/2. Dar es Salaam: IKR, kur, 46-65.
- Mulokozi, M.M na Kahigi, K.K. (1982). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. THP: Dar es Salaam.
- Mulokozi, M.M. (1989). "Uchambuzi wa Mashairi". Katika *Mulika* Na. 29, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.
- _____ (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam.
- Mutembei, A.K. (2012). *Korasi katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uhakiki*. TATAKI: Dar es Salaam.
- Samwel, M, Seleman, A.J. na Kabiero, A.J. (2013). *Ushairi wa Kiswahili: Nadharia, Maendeleo, Mwongozo kwa Walimu wa Kiswahili na Diwani ya Mea*. Dar es Salaam: MEVELI Publishers.
- Senkoro F.E.M.K. (1982). *The Prostitute in African Literature*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- _____ (2011). *Fasihi, Mfululizo wa Lugha na Fasihi Kitabu cha Kwanza*. Dar es Salaam: Washairi KAD Associates.
- Topan, F. (1974). "Dibaji ya Diwani ya *Kichomi*" ya E. Kezilahabi: Nairobi: Heinemann.

Wafula, R.M. na K. Njogu. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

_____ (2008b). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.

_____ (2010). *Kanzi ya Fasihi, Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.